

MWEZI WA RAMADHANI NA UWAZI KATIKA DHATI

Kimeandikwa na:
Sheikh Hasan Musa as-Saffar

Kimetarjumiwa na:
al-Haji Abdul-Karim Juma Nkusui

ترجمة

شهر رمضان والإنتفاح على الذات

تأليف

الشيخ حسن الصفار

من اللغة العربية الى اللغة السوا حلية

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 – 17 – 042 – 5

Kimeandikwa na:
Sheikh Hasan Musa as-Saffar

Kimetarjumiwa na:
al-Haji Abdul-Karim Juma Nkusui

Kimehaririwa na:
Al-Haji Hemedi Lubumba Selemani

Kimesomwa-Prufu na:
Al-Haji Ramadhani S. K. Shemahimbo

Kimepitiwa na:
Al-Haji Mujahid Rashid

Kimepangwa katika Kompyuta na:

Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Juni, 2016

Nakala: 2000

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation

S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640 / 2127555

Barua Pepe: alitrah@yahoo.com

Tovuti: www.ibn-tv-com

Katika mtandao: www.alitrah.info

YALIYOMO

Dibaji	1
Neno la Mchapishaji	2
Utangulizi.....	4
Mwezi wa Ramadhani na Kujichunguza	6
Wito Kuhusu Kujichunguza.....	7
Mwezi wa Kutafakari.....	8
Pande za Kutafakari	12
Mwezi wa Ramdhani na Ada za Kimakosa	16
Hakuna Uzembe na Uvivu	18
Kuondoa Matamanio ya Chakula.....	21
Kuenea kwa Kisukari na Maradhi ya moyo.....	23
Lailatul-Qadir na Maamuzi ya Kufanya Mageuzi na Mabadiliko	25

Falsafa ya Kuomba Maghofira.....	27
Nguvu ya Dua	33
Ugumu wa Maamuzi.....	34
Ni Iddi ya Upendo na Usafi na Wala sio kwa Ajili ya Ugomvi	35
Mazingira ya Ugomvi	35
Ugomvi Katika Dini.....	36
Katika Duara la Uislamu.....	40
Mtazamo wa Kifiqihi	41
Iddi ya Upendo na Usafi	43
Rejea	48

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

Sifa zote njema anastahiki Mola Mlezi wa viumbe. Ewe Mwenyezi Mungu, msalie Muhammad na kizazi cha Muhammad kama ulivyomsalia Ibrahim na kizazi cha Ibrahim, na mbariki Muhammad na kizazi cha Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na kizazi cha Ibrahim, hakika wewe ni Mtukufu Mwenye kuhimidiwa.

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ ۗ

**“Ni mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa katika (mwezi) huo Qur’an, kuwa mwongozo kwa watu na upambanuzi.”
(Surat al-Baqarah: 185).**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

DIBAJI

Kitabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kubwa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenye kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam

Al Itrah Foundation
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
SMS: +255 778 300 140

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako kimetarjumiwa kwa Kiswahili kutoka lugha ya Kiarabu. Kimeandikiwa na Sheikh Hasan Musa as-Saffar na kinaitwa, *Shahru Ramadhan wa al-Infitahu 'ala 'dh-Dhaat*. Sisi tumekiita, *Mwezi wa Ramadhani na Uwazi katika Dhati*.

Katika kitabu hiki mwandishi anaelezea falsafa ya kufunga (saumu) na faida yake katika mwili na roho.

Ni jambo la kuvutia kuona kwamba kufunga ni mojawapo kati ya ibada takriban katika dini zote isipokuwa tu utaratibu wake hutofautiana. Jambo hili limethibitishwa katika Qur'ani Tukufu kwamba ibada hii (ya saumu) haikuanzia katika Umma huu. Allah anasema katika Qur'ani Tukufu: “*Enyi mlioamini! Mmeandikiwa kufunga kama walivyoandikiwa waliokuwa kabla yenu, ili mpate kumcha Mungu.*” (2:183)

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, husasan wakati huu wa maendeleo makubwa ya kielimu ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi katika akili za watu.

Kutoka na ukweli huu, taasisi yetu ya al-Itrah imeamua kuchapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumini yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu al-Haji Abdul-Karim Juma Nkusi kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kwa lugha ya Kiswahili. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera. Amin!

Mchapishaji
Al-Itrah Foundation

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

UTANGULIZI

Jamii katika kila hatua ya mwendo wake inahitaji maarifa sahihi, yanayoionyesha uhalisia wake na yanayofungua mbele yake upeo wa matumaini na maendeleo na kuisaidia katika kukabiliana na changamoto na vikwazo. Na ili maarifa yatimize jukumu lake kwa wanajamii na yafanyie kazi nguvu zake na kunoa azma yake kuelekea kwenye maendeleo, ni lazima maarifa hayo yawe na sifa zifuatazo:

Yawe ni ya asili yanayotokana na maadili sahihi ya jamii ya ki-dini.

Yawe ya kisasa yanayoendana na mabadiliko ya maisha na mabadiliko ya kifikra.

Kutokana na maarifa hayo upatikane mpangokazi unaokidhi haja ya jamii na mahitaji yake.

Na yamiliki lugha ya kuzungumza na watu wa makundi yote na wa viwango mbalimbali, bila kuzama kwenye nadharia tupu na istihali za ubobezi zilizoenea katika hotuba za makhatibu, kwa sababu kuzungumza na watu wa kawaida kunahitaji uwezo mkubwa wa uwazi, na wa kutatua mambo halisia yaliyopo. Hivyo kundi la jamii lenye maarifa kati ya maulamaa, wanafikra na wanafasihi wao ndio upande wenye jukumu linalokusudiwa la kuzalisha na kuleta maarifa haya yanayohitajika.

Na kwa sababu hii na katika upande huu, Mwadhama Sheikh Hasan as-Safar – Mwenyezi Mungu amhifadhi – amekuwa akitoa

maarifa haya ya kukuza uwelewa kupitia uandishi, hotuba na hadhira kubwa ya kijamii.

Na silsila hii ya vitabu ni uhariri wa baadhi ya mihadhara ambayo aliitoa katika minasaba mbalimbali, na hivyo kitengo cha utamaduni katika ofisi ya Sheikh kimeandika na kuiandaa kwa ajili ya kuchapishwa hali wakitaraji kwamba itachangia katika kusambaza uelewa na kueneza fikra zenye kujenga na kustawisha maarifa katika jamii. Na wanataraji kuwa Sheikh atapata malipo na tawfiki ya ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kutoa na mmiliki wa tawfiki.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

MWEZI WA RAMADHANI NA KUJI- CHUNGUZA

Kama kila mwanadamu atajitafakari mwenyewe na kusoma maisha yake atazijua fikra alizonazo, sifa za kinafsi na utu alionao, na tabia mahususi alizonazo, na atagundua kwamba anaishi ndani ya hali na muundo unaopamba maisha yake binafsi na ya kijamii.

Na suala ambalo ni wajibu mwanadamu ajiulize mwenyewe katika nafsi yake ni:

Je, yeye yuko radhi na hali ambayo anaishi nayo?

Na je, anaihesabu nafsi yake iko katika hali nzuri na bora zaidi? Au anakabiliwa na nukta za udhaifu na mapungufu? Je, fikra alizonazo, sifa na matendo anayotenda ni jambo la lazima kwake na haiwezekani kulibadili au kuliacha? Au ni kwamba yeye ni mwanadamu ameumbwa na Mwenyezi Mungu akiwa huru, mwenye matakwa na hiyari?

Hakika maswali haya yamejificha katika nafsi ya mwanadamu mwenyewe na yanatafuta fursa ya kudhihirishwa na kufikiriwa pindi mwanadamu atakapoipa nafsi yake fursa ya kufanya hivyo, pindi atakapojichunguza na kuzama katika kina chake na kupenya katika maficho yake na mikondo yake.

Pamoja na kwamba mwanadamu ana haja kubwa ya kujidhihirisha huku, kujikagua na kujichunguza, isipokuwa watu wengi hawasimami pamoja na nafsi zao kisimamo cha kutafakari na kufunguka, hiyo ni kutokana na sababu mbalimbali, zilizo muhimu zaidi ni hizi zifuatazo:

Kwanza: Kuzama katika shughuli za kimaisha za kivitendo, nazo mara nyingi hubainika kuwa hazina thamani na umuhimu, na hudhihirika kuwa ni za kipuuzi na zisizo na maana.

Pili: Na hili ndio muhimu zaidi, ni kwamba kisimamo cha mwanadamu pamoja na nafsi yake kinahitaji kuchukua maamuzi ya kufanya mabadiliko kuhusiana na nafsi yake, na hili ndilo jambo ambalo watu wengi wanalikimbia kama ambavyo baadhi wanakimbia kufanya uchunguzi wa afya ya miili yao kwa kuogopa kugundua maradhi yatakayomlazimisha kujizuia na baadhi ya vyakula au kutumia tiba maalumu.

Wito Kuhusu Kujichunguza:

Katika mafunzo ya Kiislamu kuna wito juu ya kujichunguza na kujitathmini, na kutokuendekeza kuzama katika mambo ya kimada na shughuli za maisha ambazo haziishi. Na Imepokewa katika Hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): “Zifanyieni tathmini nafsi zenu kabla hamjahisabiwa, na zipimeni kabla hamjapimwa.”¹

Na kutoka kwa Imam Ali (as): “Ni haki ilioje kwa mwanadamu kuwa na muda usiku na mchana wa kutoshughulishwa na chochote, isipokuwa kuitathmini nafsi yake na kutizama aliyoyachuma kwa ajili ya nafsi yake na dhidi ya nafsi yake.”²

Hakika wakati wa kutafakari na kujichunguza unatoa fursa kwa mwanadamu kutambua makosa yake na nukta za udhaifu wake na kumsukuma kuiboresha nafsi yake kwa kuitoa kwenye hali duni

¹ Muhammad al-Baaqir al-Majilisiy katika Biharul- An’war, Juz. 67, Chapa ya Tatu, 1403 A.H (Beirut Darul- Ihiyaa Turathil- Islaamiy), Uk. 73.

² Abdul Wahidi al- Amadiy at Tamimiy katika Ghurartil- Hikami wa Durarul- Kalim, Chapa ya kwanza 1407 A.H (Beirut : Muasastu al- Ilimiy Lilimatubuati), Uk. 241.

kwenda kwenye hali bora zaidi. Anasema Imam Ali (as): “Matunda ya kujitathmini ni kuirekebisha nafsi.”³

Na anasema (as): “Mwenye kuifanyia tathmini nafsi yake amefaidika na mwenye kughafilika nayo amepata hasara.”⁴

Na huwenda miongoni mwa malengo ya kusimama usiku kwa ajili ya ibada ambapo mwanadamu husimama kwa hali ya kuhofu mbele ya Mola wake, katika giza na utulivu, ni kutoa fursa hii kwa mwanadamu. Vilevile ibada ya itikafu miongoni mwa hekima yake inaweza kuwa ni lengo hili, na itikafu ni kukaa msikitini kwa lengo la ibada kwa muda wa siku tatu au zaidi pamoja na kufunga, ambapo muhusika hatoki msikitini isipokuwa kwa haja ya kisharia.

Mwezi wa Kutafakari:

Haupatikani mwezi mwingine unaolingana na mwezi wa Ramadhani, ni mwezi bora ambao humo mwanadamu anasimama pamoja na nafsi yake kwa kutadaburi na kutafakari, kwani humo “Malipo huongezeka na makosa hufutwa”, kama ilivyopokelewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na katika mwezi huu kuna fursa kubwa ya kupata msamaha wa Mwenyezi Mungu: “Hakika muovu ni yule aliyenyimwa msamaha wa Mwenyezi Mungu katika mwezi huu mtukufu” kama ilivyo katika Hadithi ya Mtume (saww), na katika riwaya nyingine: “Mwenye kuudiriki mwezi wa Ramdhani na wala asisamehewe basi huyo yuko mbali na Mwenyezi Mungu.”⁵

³ Rejea iliyotangulia, Juz. 1, Uk. 323.

⁴ Sharifu Ridhaa al-Musawaiy katika Nahjul-Balagha- Qiswaaril- Kalim 208.

⁵ Muhammadiy Raishahariy katika Mizanul-Hikma, Juz. 4, Chapa ya kwanza 1402 A.H (Qum: Maktabul- I’laamil- Islaamiy), Uk. 179 – 180. Alau Diyn Ali al- Mutaqiy al-Hindi katika Kanzul- Umaal, Chapa ya tano 1405 A.H (Beirut: Muasasatu Risalah) Hadith namba 43831.

Pia imepokewa kutoka kwake (saww): “Mtu asiposamehewa katika mwezi wa Ramdhani basi ni katika mwezi gani atasamehewa?!⁶”

Na baadhi ya watu wanaweza kughafilika na kusahau kwamba kupatikana matokeo hayo kunahitajia bidii na juhudi, kwani mwezi huu unapasa kuwa ni mwezi wa kurejea, kutafakari na kuitathmini nafsi, wakati mwanadamu anapojizuia katika mwezi huu mtukufu kula, kunywa na matamano mengine yanayojitokeza kila siku, hakika anakuwa amepukana na vikwazo hivyo, jambo ambalo linampa fursa ya kuzinduka na kuitizama dhati yake na nafsi yake, na hatimaye inajitokeza hali ya kiroho ambayo imehimizwa na kukokotezwa na mafunzo ya Kiislamu ili kuboresha fursa ya kunufaika na mwezi huu Mtukufu. Swala ya usiku kwa mfano ni fursa halisi kwa ajili ya kujipwekesha na ibada pamoja na Mwenyezi Mungu, na wala haipasi kwa muumini kupitwa na wakati wa usiku kwa kulala au kwa mafungamano mengine ya kijamii na kuinyima nafsi yake nusu saa ya kuwa peke yake humo na Mola wake, baada ya nusu ya usiku, nao ndio mwanzo wa wakati wa swala hii tukufu ya mustahabu, na inapasa muumini kupanga wakati kwa ajili ya swala hii ili ilete matunda bora zaidi na matokeo yake, na aitekeleze huku akiwa katika uchangamfu na nguvu, na sio tu kwa kutimiza wajibu au mustahabu, bali lengo lake liwe kutekeleza malengo yake, amesema Mwenyezi Mungu mtukufu:

وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا

“Na katika usiku amka kwayo, ni ziada kwa ajili yako; asaa Mola Wako akakuinua cheo kinachosifika.” (Sura Israi: 79).

Na amesema (saww): “Hakika mja anapokuwa mpweke na Bwana wake katika giza la usiku na akamuomba Mwenyezi Mungu,

⁶ Kanzul- Umaal, Hadithi namba 24293.

Mwenyezi Mungu huthibitisha nuru katika moyo wake, kisha Mwenyezi Mungu mtukufu husema kwa Malaika wake: Malaika wangu tazameni mja wangu amejipwekesha kwa ajili yangu katika giza la usiku na wabatilifu wamepuuza na wameghafilika wamelala, shuhudieni hakika mimi nimemsamehe.”⁷

Na kusoma Qur’an tukufu ni jambo ambalo limehimizwa sana katika mwezi huu mtukufu, kwani ni mwezi wa Qur’an anasema (swt):

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ ۚ

**“Ni mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa katika (mwezi) huo Qur’an, kuwa mwongozo kwa watu na upambanuzi.”
(Sura al-Baqarah: 185).**

Na katika Hadithi tukufu imekuja: “Kila kitu kina msimu wa kuchanua, na kuchanua kwa Qur’an ni katika mwezi wa Ramadhani.” kama ilivyopokelewa kwamba “Mwenye kusoma humo aya atakuwa na malipo mfano wa mtu aliyekhitimisha Qur’an katika miezi mingine.”

Kusoma huku hakika kuna hudumia na kumwelekeza mwanadamu katika kuichunguza dharti yake, kuifichua na kugundua upungufu wake na makosa yake, lakini hiyo ni kwa sharti la kutafakari katika usomaji huo wa Qur’an na kuzingatia kwa kufahamu maana yake na kutazama katika upeo wa kushikamana na maamrishi ya Qur’an na kuacha makatazo yake.

Imepokea kutoka kwa Imam Ali (as) “Hakuna kheri katika kiso-mo kisichokuwa na tafakari. Tafakarini aya za Qur’an na zingatieni yaliyomo humo, hakika ni mazingatio makubwa.”⁸

⁷ Mizanul- Hikma, Juz. 5, Uk. 419.

⁸ Mizanul- Hikma, Juz. 8, Uk. 88. Kanzul- Ummal, Hadithi namba 293887.

Hakika baadhi ya watu wamezoea kusoma na kukhitimisha Qur'an mara kadhaa katika mwezi wa Ramadhani, nayo ni ada nzuri, lakini inapasa lengo lisiwe ni kumaliza kurasa tu bila ya kunufaika au kuta-fakari.

Mwanadamu anaposoma aya ya Qur'an anapaswa asimame na ajiulize juu ya msimamo wake kwa yale inayoyasema aya hiyo, ili atoe fursa ya kuathirika katika moyo wake na kwa ajili ya mabadiliko katika moyo wake na nyendo zake. Imepokewa kutoka kwa Mtume (saww): "Hakika nyoyo hizi zinapata kutu kama kinavyopata kutu chuma." ikasemwa: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu tutawezaje kuitakasa? Akasema: "Kwa kusoma Qur'an."

Na kwa hiyo mwanadamu anatibu maradhi ya nafsi yake na upungufu wa shakhisiya yake, kwani Qur'an ni ponyo kwa yaliyomo katika nyoyo.

Na dua zilizopokelewa katika mwezi wa Ramadhani kama vile dua ya Ifitaahi, dua ya Sahri na dua za mchana na usiku wa mwezi wa Ramadhan zote ni hazina ya malezi ya kiroho, zinamletea mwanadamu ushujaa katika kurekebisha dhati yake na kuichunguza nafsi yake, na zinanoa azma yake na matakwa yake kwa ajili ya mabadiliko na mageuzi na kumhimiza kutubia madhambi na makosa. Kama ambavyo zinatia mkazo katika nafsi yake utukufu wa Muumba na umuhimu wa hatima yake, na kuiweka mbele ya ukweli na uwepo wake na uhalisia wake bila ya kuwa na pazia.

Na mwanadamu anaposoma dua kama vile dua ya Sahri ambayo ameipokea Abu Hamza Thumaaliy (r.a) kutoka kwa Imam Zainul-Abidin (as) hakika ni juu yake azingatie vipengele vya dua, kuwa vinaelezea yaliyo katika nafsi yake yeye mwenyewe, na sio asome kana kwamba ni maelezo ya mtu mwingine kwa Mola wake.

PANDE ZA KUTAFAKARI

Hakika kitendo cha mwanadamu kutafakari na kurejea kina umuhimu mkubwa katika pande tatu:

Upande wa kwanza: Kurejea katika fikra:

Mwanadamu arejee fikra zake na imani yake na ajiulize juu ya kiasi cha haki na usahihi wake, na lau kama watu wote wangerejea fikra zao na ufuasi wao pengine wangeweza kubadili makosa na upotovu uliyopo katika imani zao, isipokuwa uhalisia wa watu wengi ni **“Hakika sisi tumekuta baba zetu katika desturi na sisi tunafuata nyayo zao.”** Na mwanadamu anapasa awe huru na nafsi yake, mwenye nguvu katika dhati yake, anapogundua kwamba yuko katika kosa fulani, basi asiogope au asisitesite kubadilika na kusahihisha.

Upande wa pili: Kuirejea nafsi:

Mwanadamu arejee sifa za nafsi yake ambazo humo imefichikana shakhisiya yake, je ni mwoga au ni shujaa? Ni jasiri au ni mwenye kusitasita? Ni shupavu au ni dhaifu? Mkweli au muongo? Muwazi au msiri? Mvivu au mchapakazi? Mwanadamu aulize katika nafsi yake idadi ya maswali ambayo yanafichua upande huu, mfano: Nita-fanya nini kama atanijia fakiri katika nyumba yangu? Nita-fanya nini kama watoto wangu watachezea samani za nyumba? Nita-fanya nini kama kutatokea mbele yangu ajali? Na jibu langu litakuwaje kama nitakosewa mbele ya watu? Na nitaamua nini kama maslahi yangu binafsi yatagongana na dini au maslahi ya umma na jamii?

Na umuhimu wa kujirejea huku unajitokeza kwa sababu mwanadamu baada yake anapasa arekebishe kila upungufu wa kinafsi

uliyopo kwake, na afanye kazi ya kuboresha nafsi yake na kuisogeza hatua zaidi mbele.

Upande wa tatu: Kurejea katika jamii na tabia

Mwanadamu arejee nyendo zake na vitendo vyake dhidi ya wengine, kwa kuanzia na mke wake watoto wake na kumaliza na watumishi wake na wafanyakazi wake na kwa jamaa zake na marafiki zake na watu wengine kati ya anaamiliana pamoja nao au anaofungamana nao.

Na mwezi huu mtukufu ni mnasaba bora wa kupanda daraja kwa utekelezaji wa kijamii kwa muumini, na kuondoa ikhitalafu zote, kasoro za kijamii na mifundo binafsi baina ya mwanadamu na wengine, riwaya nyingi zimehimiza juu ya hilo kiasi kwamba baadhi ya riwaya zinaeleza: Kwamba maghofira ya Mwenyezi Mungu na msamaha wake kwa mwanadamu unabakia umening'inia kwa muda mrefu hadi aondoe yaliyo baina yake na wengine miongoni mwa ikhitalafu na kuwa mbali, hata kama wao ndio wakosaji katika haki yake, katika hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Imam Ridha (as) amesema: “Katika usiku wa kwanza wa mwezi wa Ramadhani wanafungwa waasi miongoni mwa mashetani na wanasamehewa kwa kila usiku watu sabini elfu, na unapofika usiku wa Lailatul-Qadir Mwenyezi Mungu husamehe mfano wa aliyosamehe katika mwezi wa Rajab, Shaaban na mwezi wa Ramadhani hadi siku hiyo, isipokuwa mtu ambaye baina yake na ndugu yake kuna ugomvi, atasema (swt): Waacheni hawa hadi wasuluhishane.”⁹

Hata kama mmoja wao ni dhalimu na mwingine ni mwenye kudhulumiwa hakika wao kwa pamoja wanabeba dhambi ya kuhama na kutengana, ambapo mwenye kudhulumiwa kati yao anaweza kumwanza ndugu yake kwa kusamehe na kuondoa ikhitalafu, katika

⁹ Mizanul- Hikma, Juz. 11, Uk. 414.

hadithi kutoka kwa Imam al-Baqir (as) amesema: “Hakuna waumi-ni wawili wanaotengana zaidi ya siku tatu isipokuwa watatengwa mbali (na Allah).” Akaambiwa: Ewe mjukuu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu: Hii ni katika hali ya mwenye kudhulumu, lakini vipi mwenye kudhulumiwa? Akasema (as): “Na kwanini mwenye kudhulumiwa haendi kwa dhalimu na kusema: Mimi ndio dhalimu ili wasuluhishane.”¹⁰

Ni uwazi ulioje katika wito wa suluhu ya kijamii, na ni utukufu ulioje wa matokeo kama utatimia ndani ya mwezi huu mtukufu, na ni ukubwa wa cheo ulioje wa nyoyo hizo ambazo zinaweza kumaliza ikhitilafu zake na kusuluhishana katika mwezi wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kupata msamaha wa Mwenyezi Mungu? Hapa hakika mwanadamu anahitaji moyo safi uliotakasika na nia ya kheri na ya kweli kama alivyosema (saww): “Muulizeni Mola wenu kwa nia za kweli na nyoyo safi.”

Pongezi kwa mwenye kunufaika na mazingira ya mwezi huu mtukufu kwa kufunguka na kuwa muwazi juu ya dhati yake, na kurekebisha makosa yake na aibu zake na kuziba mapungufu yake na dosari katika shakhisiya yake, na kurejea fikira zake na rai zake na kuzidurusu kimaudhui, na anatafakari sifa zake za kinafsi ili aone nukta za nguvu na udhaifu humo, na kutafiti nyendo zake za kijamii kwa ajili ya kujenga uhusiano bora zaidi pamoja na wanaomzunguka.

Na kwa kurejea huku na kuacha makosa unapatikana msamaha wa Mwenyezi Mungu mtukufu kwa mwanadamu katika mwezi wa Ramadhani, ama mwanadamu akibakia na akiendelea na bumbuwa-zi katika mazingira yake na hali yake hakika ataikosha nafsi yake fursa hii kubwa, na utamalizika mwezi wa Ramadhani bila ya kua-

¹⁰ Rejea iliyotangulia Uk. 315.

cha alama yenye kuathiri katika shakhisiya yake na tabia yake, na kisha atainyima nafsi yake msamaha wa Mwenyezi Mungu mtukufu, na yatasadikika kwake aliyoyasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): “Hakika muovu ni yule aliyenyimwa msamaha wa Mwenyezi Mungu katika mwezi huu mtukufu.” “Hakika asiyenufaika na fursa hii wala hafaidiki na mazingira haya mazuri atakuwa ni muovu.”

MWEZI WA RAMADHANI NA ADA ZA KIMAKOSA

Mwezi mtukufu wa Ramdahani ni sehemu na muda bora sana unaompitia mwanadamu ndani ya mwaka ambapo Mwenyezi Mungu ameufanya ni mahususi kwa kheri na fadhila ukilinganisha na muda na wakati mwingine, na akajaalia humo Lailatul-Qadir ambao ni usiku bora kuliko miezi elfu moja, na akauchagua ili uwe shukio la wahyi wake na ujumbe wake ambapo humo aliteremsha Qur'an na kabla ya hapo humo ilishuka Taurati, Injili na Zaburi.

Na inatosha katika ubora wa mwezi huu yaliyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): “Bwana wa miezi ni mwezi wa Ramdahani.”¹¹

Na kutoka kwake (saww): “Enyi watu hakika umekujieni mwezi wa Mwenyezi Mungu kwa baraka, rehema na maghofira, ni mwezi ambao ni bora sana kwa Mwenyezi Mungu kuliko miezi mingine, na siku zake ni siku bora sana, na mikeshi yake ni mikeshi bora sana, na saa zake ni saa bora sana, ni mwezi ambao humo mmealikwa katika ugeni wa Mwenyezi Mungu, na humo mkajaaliwa kuwa ni watu waliokirimiwa na Mwenyezi Mungu.”¹²

Na kwa kutia mkazo mahususi na kwa kuupambanua mwezi huu mtukufu Mwenyezi Mungu amefaradhisha fungu yake kwa watu ili waishi humo kwa mazingira na ratiba ya kipekee inayowasaidia wao kunyanyuka kwa cheo cha mwezi huu na nafasi yake tukufu.

¹¹ Kanzul- Ummal, Juz. 463 Hadith namba 23670

¹² Biharul- An'war, Juz. 93, Uk. 356

Na saumu ina faida na manufaa makubwa, katika upande wa kiafya saumu inaleta raha ya kifiziyojia katika viungo vya mwili miongoni mwa kazi ya kumeng'anya chakula, kama ambavyo inatoa fursa ya kumeng'anya kilichokusanywa humo, na kuondoa sumu iliyorundikana humo, na kurahisisha kazi ya mabadiliko ya kimaisha, na kwa sababu hiyo sasa hivi jopo la matabibu linazingatia na kusisitiza kile kinachoitwa 'funga ya kitabibu' na wametoa msembo wa kitabibu ambao unatibu mvurugiko wa kimwili na baadhi ya maradhii yake sugu, na vimetungwa kuhusu hilo vitabu vingi vya kielimu kama vile kitabu cha *Atadaawiy Biswaum* mtunzi wake ni H. M. Shiyilton, ambacho kimetarjumiwa kwa lugha ya kiarabu na kimesambazwa mwaka 1987 na Daru Rashid- Damascus na Beirut.

Na katika upande huu wa kinafsi hakika kuna semina ya mafunzo ya kumlea mwanadamu katika kudhibiti raghaba zake na matamania yake, ambapo anajizuia kwa maamuzi ya dhiti dhiti ya kula na kunywa na vifunguzi vingine tena kwa utashi wake mwenyewe huku akiwa na haja navyo katika baadhi ya nyakati. Na kijamii mwanadamu anahisi kupitia saumu njaa ya mafakiri na wasionacho, na anahisi mateso yao na haja zao.

Na kiroho hakika kujiepusha na raghaba na kuamiliana na mazingira matukufu ya mwezi mtukufu wa Ramadhani kunazalisha utakaso wa kiroho na uchangamfu wa kimaanawi wa hali ya juu.

Lakini faida hizi na manufaa haya na mfano wake hakika yanapatikana pale tu panapokuwa na uelewa sahihi juu ya saumu na kuwa tayari kutoa fursa kwa faradhi ya saumu tukufu, na kwa kuheshimu mazingira ya Ramadhani tukufu, kujituma na kuleta athari zake bila ya vikwazo na hali pinzani za kinyume chake.

Na jambo ambalo linasikitisha ni kuenea na kusambaa kwa baadhi ya ada za kimakosa na hali mbaya ambazo zinatengua athari za

saumu na kupunguza manufaa na baraka za mwezi mtukufu, hapa tunaangazia juu ya hali mbili mbaya zinazosambaa aghlabu ndani ya wenye kufunga na kuwanyima wao manufaa yanayotakiwa ya mwezi huu mtukufu.

Hakuna uzembe na uvivu:

Mwanadamu anapomiliki wakati ghali na muhimu hakika ni juu yake autumie katika amali bora na ratiba sahihi, na sio aupoteze katika upuuzi na mambo yasiyo na manufaa. Mwezi wa Ramadhani ni mwezi bora na fursa ya muda ghali sana unaopita kwa mwanadamu katika ulimwengu hivyo inapasa achunge kila saa kati ya saa zake na sekunde kati sekunde zake kama ilivyopokewa kutoka kwa Mtume wa Mwezi Mungu (saww): “Siku zake ni siku bora kabisa, na mikesha yake ni mikesha bora kabisa na saa zake ni saa bora kabisa.”

Na maana ya hayo ni kwamba inapasa kusherehekea mwezi wa Ramadhani kwa ratiba bora na vitendo vyema na uzalishaji wa mwanadamu humo uwe mwingi zaidi na harakati zake ziwe kubwa zaidi.

Na hivyo tunaona mafunzo ya Kiislamu yanatoa ratiba nyingi ya vitendo vya ibada katika mwezi wa Ramdhani:

1. Kuna nyuradi na swala nyingi za mustahabu
2. Dua mbalimbali za mchana na mikesha ya mwezi huu. Anasema Imam Ali (as): “Ni juu yenu katika mwezi wa Ramdhani kuzidisha istighfari na dua.”
3. Na ni mustahabu kuzidisha kusoma Qur’an kama ilivyopokewa katika hadithi kutoka kwa Imam al-Baqir (as) “Kila kitu kina msimu wake na msimu wa Qur’an ni mwezi wa Ramadhani.”

Na katika nyanja za kijamii kuna maelekezo ya kidini ya kuzidisha shughuli za kijamii katika mwezi wa Ramadhani kama tuna-vyosoma katika hotuba ya Mtume wa Mwezi Mungu (saww) katika mwezi huu mtukufu ambapo anasema:

“Na toeni sadaka kwa mafakiri wenu na maskini wenu, waheshimuni wakubwa wenu, wahurumieini wadogo wenu na ungeni udugu wa jamaa zenu, wahurumieni mayatima wa wengine watahurumiwa mayatima wenu.”¹³

“Mwenye kumfuturisha muumini aliyefunga miongoni mwenu katika mwezi huu kwa hilo atakuwa na malipo kwa Mwenyezi Mungu sawa na ya mtu aliyemwacha huru mtumwa na kusamehewa yaliyopita katika madhambi yake.”¹⁴ Na katika hadithi nyingine: “Mwenye kumfuturisha mfungaji atakuwa na mfano wa malipo yake.”¹⁵

Riwaya hizi na mfano wake zinamaanisha mwanadamu awe na ratiba nyingi ndani ya mwezi wa Ramadhani katika upande wa ibada na nyanja za kijamii, wakati wa mwanadamu humo uwe umesheheni kwa uchangamfu na harakati nyingi kwani ni mwezi wa uchangamfu, harakati na amali.

Lakini mambo ambayo wameyazoea walio wengi katika jamii zetu ni kuufanya mwezi huu kuwa ni msimu wa uvivu na uzembe, ambapo unashuka humo ufundishaji katika madrasa, utendaji kazi katika maofisi na taasisi, sehemu kubwa miongoni mwa watu humo wanamaliza mchana wao kwa kulala na kupumzika kwa hoja ya funga kana kwamba saumu ndio sababu ya uvivu au badala ya kazi, mwanadamu anasimamisha harakati zake ili afunge, na utaona ka-

¹³ Muhammad bin Hasan al-Huruli al-Miliy katika Wasailu Shia Juz. 10, Chapa ya kwanza 1993 (Beirut muasasatu lihiyai turaathi) Uk. 313, Hadithi namba 20 – 13494.

¹⁴ Rejea iliyotangulia.

¹⁵ Muhammad bin Isa Tirimidhiy katika Sunan Tirimidhiy, Juz. 1, Chapa ya kwanza 1421 A.H (Beirut Darul kutubil- ilimiya), Uk. 567, Hadithi 807.

tika baadhi ya ripoti kushuka kwa kiwango cha uzalishaji wa kikazi katika sehemu ya jamii za Kiislam katika mwezi wa Ramdhani.

Na katika historia yetu ya Kiislam mwezi mtukufu wa Ramdhani ulikuwa na vita nyingi miongoni mwa vita vya ushindi baina ya Waislamu na makafiri, na Waislamu wamepata humo ushujaa na ushindi, vita ya Badri kubwa ilitokea katika mwanzo wa mwezi wa Ramadhani ambapo Mwenyezi Mungu alifaradhisha saumu yake katika mwaka wa pili Hijiria, na Ukombozi wa Mji wa Makka ulitokea katika mwezi wa Ramadhani katika mwaka wa kumi Hijiria, na katika mwezi wa Ramdhani Waislamu walifungua kisiwa cha Rhodes mwaka wa 53 Hijiria, kama ambavyo walifungua mpaka wa Hispania chini ya ujemedari wa Musa bin Nadhir mwaka 91 Hijiria.

Na ni katika mwezi huo Wakristo wa Kifaransa ambao waliitaka Syria na pembezoni mwake walishindwa chini ya jeshi la Waislamu mwaka 584 Hijiria.

Na baba zetu na mababu zetu walikuwa wanafunga mwezi wa Ramadhani pamoja na kufanya kazi zao za kimaisha, kazi hazikuwa zinasimama katika nchi zetu katika muda wa saumu. Vipi imetokea hali hii mbaya ya kutawaliwa na uzembe na uvivu kwa walio wengi mchana wa mwezi wa Ramadhani.

Hakika kuhuisha mikesha ya mwezi wa Ramadhani kwa ibada na amali za kheri ni jambo zuri lakini walio wengi wanakesha usiku katika vikao vya kipuuzi au katika ratiba zisizo na manufaa, ni kupitisha wakati tu kisha wanatumia mchana mwingi kwa kulala badala ya kufanya kazi ya uzalishaji.

Na katika upande wa kiafya hakika kulala wakati wa funga kunadhoofisha mwili na kuuzuia kunufaika na saumu, ripoti za kitabu zimetaja: Kwamba harakati za viungo katika muda fulani baada ya kufyonza chakula – wakati wa funga – huchangamsha kazi ya

oksidisho (oxidation) ya virutubisho ambavyo vinauongezea mwili nguvu na vinafanya kazi ya kuyeyusha mafuta, kama ambavyo vinafanya kazi ya kutengeneza glukosi katika ini, katika glyserini inayotokana na kuyeyusha mafuta katika njia ya mishipa na katika laktosi inayotokana na oksidisho (oxidation) ya glukosi katika viungo.

Na kitabu *Swiyaamu Muujizatu Ilimiyah* cha Dr. Abdul- Jawad Swawiy, kimejaa utafiti mzuri wa kielimu kuhusu maudhui haya chini ya anwani: Ni ipi hali bora wakati wa saumu, ni kufanya kazi au kutulia?¹⁶

Zaidi ya hapo ni kwamba kulala mchana kwa mfungaji huondosha malengo mengi ya saumu, kwani hatohisi njaa wala kupatwa na raghaba wala matamano, namna gani na ni wakati gani itasadiki kwa mfungaji aliyelala kwamba anaonja makali ya njaa na kuhisi adha ya wasionacho au anajiepusha na matamano yake na raghaba zake, na hivyo kukua hali ya uchamungu wakati yeye amelala?

Na ikiwa mwanadamu mwaka mzima anakula na kunywa mchana na anajizua kula na kunywa wakati wa kulala kwake usiku, hakika katika hali hii anakuwa amebadili ratiba yake, kwa sasa anakula na kunywa wakati wa usiku na anajizua kula na kunywa wakati wa mchana naye amelala, sasa kuna tofauti gani?

Kuondokana na Matamano ya Chakula:

Miongoni mwa faida dhahiri ni malezi ya mwanadamu katika kudhibiti matamano ya kula. Hiyo ni kwa sababu kuna viwango viwili katika mwanadamu kula chakula.

Kiwango cha kwanza: Haja ya mwili kwenye chakula, kwa sababu kimetengenezwa na chembechembe za sehemu za ardhi: udongo,

¹⁶ Dr. Abdul- Jawad Swawiy katika *Swiyaam Muujizatu Ilimiya* chapa kwanza 1413 hijria (Jidda Darul Qiblata islamiya), Uk. 114 – 123.

maji na hewa, na Mwenyezi Mungu amedhalilisha mimea na wanyama kama chakula cha mwanadamu, unakua mwili wake kwa vitu hivi na virutubisho hivi ili maisha yake yaendeleo na kustawi kwake, na inatosha katika kutimia lengo hili kwa kiwango kidogo cha chakula kama ilivyokuja katika hadithi: “Inamtosha mwanadamu tonge chache zinazoimarisha mgongo wake.” Kama ilivyopokewa kutoka kwa Nabii (saww).¹⁷

Kiwango cha pili: Hali ya raghaba na matamania, ambapo mwanadamu anaburudika kwa ladha ya chakula na zinamtamania aina zake mbalimbali, anakula kwa raghaba hii kwa kuvuka mahitaji ya mwili wake, bali anaweza kula yale ambayo yanadhuru mwili wake kwa idadi na aina.

Hapa mwanadamu anatoftiana na mnyama ambapo matamania yao yanafungamana na haja ya mwili wake na kwa hali ambayo imedhalilishwa kwake, ama mwanadamu matamania yake yana upeo mpana zaidi kulingana na mahitaji yake, kama atayakubalia na akaendelea katika kula na kunywa, hakika hiyo itamsababishia maradhi na magonjwa.

Hivyo tiba inahadharisha kuzidisha chakula na kutokuwa na wastani katika chakula, kama ambavyo inatia mkazo juu ya mafunzo hayo ya kidini, imepokewa kutoka kwa Mtume (saww): “Jihadharini na kuzidisha vyakula hakika kunatia sumu moyo.” Na anasema Imam Ali (as): “Mwenye kuzidisha kula inadhoofika afya yake.”¹⁸

Na matatizo mengi ya kiafya ya mwanadamu yanatokana na kundenkeza matamania ya kula na kunywa, na hususan katika zama hii ambayo humo kuna ushindani wa njia za propaganda na matangazo yanayoshajiisha matumizi, na viwanda na mahoteli ya vyakula yanaenda mbio kuchochea raghaba za watu zaidi katika aina ya vyaku-

¹⁷ Biharul- An'war, Juz. 63, Uk. 329

¹⁸ Mizanul- Hikma, Juz. 1, Uk. 117 -118.

la vinavyozalishwa, kama ambavyo mazingira ya maisha kwa walio wengi hayalazimu kutumia juhudi na harakati ili kutumia nguvu ambayo inatengenezwa na vyakula katika mwili.

Na inakuja fursa ya saumu ili mwanadamu atazame dharura ya kudhibiti chakula chake na vinywaji vyake na kudhibiti raghaba yake na matamano yake, lakini yanayosikitisha sana ni yale ambayo yanatawala maisha ya jamii zetu nyingi, ambapo kinaongezeka kiwango cha matumizi ya chakula katika mwezi wa Ramadhani, na kulingana na baadhi ya ripoti za uchumi, hakika matumizi ya dola za Kiislamu ya vyakula kinaongezeka katika mwezi wa Ramadhani.

Mwezi mtukufu umekuwa ni msimu wa vyakula na kuongezeka kwa raghaba ya chakula, na unapowadia wakati wa kufuturu mwanadamu anaelekea kwenye meza ya kulia chakula kwa raghaba na uroho kana kwamba analipiza kisasi katika tumbo lake kutokana na muda wa saumu yake.

Kuenea kwa Maradhi ya Kisukari na Moyo:

Katika jamii zetu na ambapo uchumi ni mzuri na kwa kuendekeza matamano na raghaba, tumekuwa tunakabiliwa na hali ya kuenea kwa baadhi ya maradhi hatari ambayo aghlabu yanatokana na kutojidhibiti katika ratiba ya chakula.

Ilitangazwa katika mkutano wa kisukari duniani ambao ulifanyika mara ya mwisho Cairo, kwamba Saudia inaongoza katika orodha ya nchi ambazo humo yameenea maradhi ya kisukari, baada ya kuwakuta watu 900,000 wakiwa na maradhi ya kisukari katika Saudia, yaani wastani wa asilimia kumi na saba (17%) ya wakazi wa Saudia.

Kama ambavyo kongamano la tiba lililofanya mkutano wake wa mwisho huko Dhaharani kwa anwani ya ‘Kisukari wigo wa mustakabali’ utafiti wake uliashiria ongezeko la matatizo yatokanayo na

maradhi ya kisukari, kama vile kuzidi kwa kilo, shinikizo la damu, maradhi ya moyo na kukatika kwa viungo.

Katika mwaka mmoja umefanyika upasuaji mara 13 elfu wa kukata viungo katika nchi ya Saudia kwa sababu ya kisukari, na Riyadh peke yake hufanyika upasuaji mara 36 wa kukata viungo kwa siku, nacho ni kiwango cha juu katika wastani wa kiulimwengu.

Na inaonyesha ripoti ya mwaka inayotolewa na chama cha afya cha kimataifa kwamba wastani wa ziada wa kila mwaka wa maradhi ya kisukari katika Saudia kiwango chake ni asilimia 4, yaani watu wapya 36,000 kila mwaka wanapatwa na kisukari katika Saudia!! Na sehemu ya Mashariki ndio inayoongoza kwa kupatwa na maradhi haya.¹⁹

Na sambamba na maradhi ya kisukari kuna ongezeko la kuenea maradhi ya moyo ambayo aghlabu yanatokana na kuzidi kiasi cha lehemu na mafuta katika mwili wa mwanadamu.

Hakika ni juu yetu tujiulize: Je, sisi tunaishi ili tule au tunakula ili tuishi? Ikiwa chakula ni kwa ajili ya maisha basi tudhibiti chakula ili tunufaike na faida kubwa ya saumu.

¹⁹ As shariq: tolea la 999, Uk. 14.

LAILATUL – QADIR: MAAMUZI YA MAGEUZI NA MABADILIKO

Mwenyezi Mungu anasifia usiku wa Lailatul- Qadir kwamba ni bora kuliko miezi elfu moja, na kwamba ndani ya Lailatul- Qadir huhukumwa kila jambo jema, ambapo yanapangwa matukio, makadirio na mambo ya hatima ambayo yanafungamana na mwanadamu na maisha katika usiku huu kutoka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu.

Kutoka kwa Ibnu Abbasi: “Hakika Mwenyezi Mungu anakadiria yatakayokuwa katika mwaka huo miongoni mwa mvua, riziki, kuhuisha na kufisha, kuanzia usiku huo hadi mwaka ujao.”²⁰

Na kutoka kwa Imam Ali bin Musa Ridhaa (as): “Lailatul- Qadir, Mwenyezi Mungu mtukufu anakadiria humo yatakayokuwa mwaka hadi mwaka (ujao) miongoni mwa kuhuisha au kufisha au kheri au shari au riziki.”²¹

Hivyo Lailatul – Qadir ni usiku wenye cheo kwa Mwenyezi Mungu kwa kukadiria ambayo yatatokea kwa watu katika mwaka wao unaokuja, na ni usiku wa maamuzi makubwa ya Mwenyezi Mungu, hivyo basi usiku huu uwe ni usiku wa maamuzi muhimu kwa mwanadamu.

Ni taufiki tukufu ilioje na yenye thamani kubwa, mwanadamu kupanga ratiba kwa ajili ya nafsi yake, kufanya maamuzi ya hatima yake ya kimsingi, katika usiku huo mtukufu ambao Mwenyezi Mungu mtukufu amejalia kuwa ni muhula na wakati wa makadirio yake kwa mwanadamu.

²⁰ Al-Fakhar Raaziy katika fafsir al- kabiir, Juz. 32, Chpa ya kwanza 1418 A.H (Beirut Muasasatu Daril- Islami), Uk. 28

²¹ Abdu Ali bin Jumu’ a al- Arusiy al- Jariry katika tafsir Nuru Thaqaalain, Juz. 5, Chapa ya kwanza 1422 A.H (Beirut Muasastu Tarikhil- Arabiy), Uk. 630.

Kisha yanakuja mazingira ya kiroho matukufu ambayo yanazunguka usiku huu, ili kuzidisha hadhi ya mwanadamu kufanya maamuzi ya kimaisha yenye msimamo sahihi.

Na hakuna shaka kwamba duara la maamuzi ya mwanadamu katika usiku huu mtukufu linapasa lipanuke kiasi cha kujumuisha kila lenye dauru, mchango na athari katika msimamo wake na maslahi yake, na lijumuishe mategemeo ya mwanadamu ya kidunia na ya Akhera. Aiwekee nafsi yake mipango na ratiba ya kivitendo na kitabia na kuifuata katika mwaka wake unaokuja kisha amwahidi Mwenyezi Mungu katika usiku huo, bali na katika mikesha yote ya Lailatul- Qadiri kuwa ataendelea kutekeleza ratiba hiyo, na aombe nguvu na msaada kwa Mwenyezi Mungu na ajaalie hukumu yake na makadirio yake yaafiki matamanio yake na matarajio yake mema.

FALSAFA YA KUOMBA MAGHOFIRA

Hakika moja ya amali muhimu sana katika usiku huu ni kuomba maghofira kwani imepokewa kuwa katika suna za usiku huu ni mtu aombe maghofira kwa Mwenyezi Mungu mara sabini.

Na kutoka kwa Amirul-Muuminina Ali (as) kwamba amesema: “Ni juu yenu katika mwezi wa Ramadhani kuzidisha kuomba maghofira na dua, ama dua inazuia balaa kwenu, ama kuomba maghofira kunafuta dhambi zenu.”²² Na Nabii mtukufu (saww) anamlaumu mwenye kuinyima nafsi yake kupata msamaha wa Mwenyezi Mungu katika mwezi huu mtukufu kwa kauli yake (saww): “Muovu ni yule mwenye kunyimwa msamaha wa Mwenyezi Mungu katika mwezi huu mtukufu.” Na anasema: “Mwenye kuudiriki mwezi wa Ramadhani na asisamehewe basi Mwenyezi Mungu amuweke mbali.” Na pia amesema (saww): “Ambaye hajasamehewa katika mwezi wa Ramadhani basi ni katika mwezi upi atasamehewa?”

Na Ramadhani sio tu ni madrasa ya kiroho bali pia ni semina ya malezi, humo anahitimu mwanadamu kwa kujipamba na mambo mema na mafanikio ili ayatumie katika mwaka wake uliobakia, hapa ndipo maelekezo ya Kiislamu yanaonesha dharura ya kuomba maghofira kwa wingi, na yanatia mkazo juu ya umuhimu huo katika maisha yote ya mwanadamu.

Anasema Mtume (saww): “Zidisheni kuomba maghofira hakika Mwenyezi Mungu mtukufu hajakufundisheni kuomba maghofira isipokuwa naye anataka kuwasameheni.”²³ Na amesema Imam as-Sadiq (as): “Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa anatubia

²² Wasailu shia, Juz. 10, Uk. 304.

²³ Mizanul- Hikma, Juz. 7, Uk. 247.

kwa Mwenyezi Mungu katika kila siku mara sabani bila ya kufanya dhambi.”²⁴

Hakika kuomba maghofira ya kweli sio kusema tu *Astaghafirullahi* na kutikisa ulimi kwa matamko haya bali matamko haya yana-pasa yawe ni alama dhahiri ya maamuzi ya msingi na ya kina katika nafsi ya mwenye kuomba maghofira.

Hakika uhalisia wa kuomba maghofira kwa hakika unatakiwa upitie hatua mbili muhimu za kimsingi:

Kwanza: Kugundua kosa, na kukiri uwepo wake, na kwamba ni kosa haijuzu kuendelea nalo.

Pili: Kuazimia juu ya kuling’oa na kuepukana nalo.

Unapojua kosa na kulianisha kisha ukaazimia kuliepuka na kuling’oa wakati huo ndio utangaze maamuzi yako hayo ya moyoni, kwa ulimi wako na kusema: “*Astaghafirullahi Rabbii waatubu ilaihi.*”

Hakika kuomba maghofira kwa maana hii kunageuka kutoka kwenye dhikiri tu, na kuhama kiaina na kuelekea katika hali bora na sahihi na inakuwa ni dawa ya maradhi ya mwanadamu na ugonjwa wake, anasema (saww): “Je, niwaonyesheni ugonjwa wenu na dawa yenu? Fahamuni hakika ugonjwa wenu ni madhambi na dawa yenu ni kuomba maghofira.”²⁵ Na kama tukimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): “Ni aina gani hii ya kuomba maghofira ambayo unaiielezea kwetu ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Atasema kama ilivyo katika hadithi iliyopokelewa kutoka kwake (saww): “Aina bora ya kuomba maghofira kwa Mwenyezi Mungu ni kung’oa (dhambi) na kujuta.”²⁶

²⁴ Wasailu Shia, Juz. 16, Uk. 85, Hadithi 21047.

²⁵ Mizanul- Hikma, Juz. 7, Uk. 247.

²⁶ Rejea iliyotangulia Juz. 7, Uk. 255.

Ama ikiwa kuomba maghofira ni kutikisa ulimi tu, wala hakufichui azma yoyote ya kung’oa dhambi, hakika – hali ikiwa ndio hii - inageuka kuwa dhambi anayoadhibiwa kwayo mwanadamu; na ni kauli nzuri ilioje ya Imam Ali (as) katika kuashiria ukweli huu ali- posema: “Kuomba maghofira pamoja na kung’ang’ania madhambi ni kuyaongeza upya.”²⁷ Hiyo ni kwa sababu kuomba maghofira kwa namna hii ni sawa na ahadi ya kauli isiyo na shaka pamoja na kua- zimia kwa ndani kutoitimiza, na Mwenyezi Mungu mtukufu anajua yaliyomo katika nafsi yako.

Na anasema Imam Ali Ridhaa (as) katika neno zuri: “Mwe- nye kutaka maghofira kwa ulimi wake na wala hakujuta kwa moyo wake basi ameichezea shere nafsi yake.”²⁸ Na anasema (as) ka- tika hadithi nyingine: “Mwenye kuomba maghofira katika dhambi anayoendelea kuifanya ni sawa na yule anayemchezea shere Mola wake.”²⁹

MAAMUZI YA MAGEUZI NA MABADILIKO

Hakika kila mwanadamu anakabiliwa na makosa na wala hanu- suriki na shimo hilo isipokuwa aliyehifadhiwa na Mwenyezi Mungu mtukufu:

وَمَا أُبْرِيْ نَفْسِيْ ۚ إِنَّ النَّفْسَ لَأَمَّارَةٌ بِالسُّوْءِ ۗ إِلَّا مَا رَحِمَ رَبِّي ۚ إِنَّ رَبِّي غَفُوْرٌ
رَّحِيْمٌ

“Nami sijitakasi nafsi yangu; hakika nafsi ndiyo iamrishayo mno uovu, isipokuwa ile ambayo Mola Wangu ameirehemu. Hakika Mola

²⁷ Rejea iliyotangulia

²⁸ Rejea iliyotangulia

²⁹ Rejea iliyotangulia

**Wangu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.”
(Sura Yusuf: 53).**

Na taufiki ni mwanadamu kuzinduka kwa ajili ya nafsi yake kwamba anapita katika kosa fulani, na kwamba bado hajapata taufiki ya kufikia kwenye ukamilifu kati ya ukamilifu mtukufu, na huu ndio mwanzo wa taufiki ya Mwenyezi Mungu ambapo ndio nukta ya mageuzi kuelekea kwenye uongofu, anasema (saww): “Hakika kila binadamu ni mwenye kukosea na wakosaji bora ni wale wenye kutubia.”³⁰

Na hapa mwanadamu anahitaji kuwa muwazi sana pamoja na nafsi yake kwa ajili ya kusahihisha kosa, na ajiulize namna gani nitaweza kung’oa dhambi zangu na namna gani ninaweza kubadilisha makosa yangu na mapungufu yangu?

Na unazidi umuhimu wa kujigundua na ukubwa wa umuhimu wote kila kosa linapogeuka na kuwa ni mazoea, hiyo ni kwa sababu mazoea ni tabia nyingine, na mazoea kwa kila mwanadamu ni mta-wala, na kwa hiyo mazoea yanageuka kuwa ni mgomvi mwenye kushinda kwa mwanadamu, mazoea ni yenye kuteza nguvu kama ilivyo katika maelezo ya Amirul-Muuminina Ali bin Abi twalib (as).³¹

Na kuomba maghofira ni kuazimia kufanya mabadiliko kwa kuachana na tabia ya kimakosa hata kama itageuka na kuwa mazoea aliyoyazoea mwanadamu kwa muda mrefu.

Na huwenda kuna ugumu katika jambo, lakini aliyompa Mwenyezi Mungu mwanadamu miongoni mwa matakwa, azma, akili na uwezo wa kuchagua, yote hayo yanampa mwanadamu ushindi dhidi ya mapungufu yake na makosa yake.

Ni sahihi kwamba taufiki ya Mwenyezi Mungu ni lazima ipatikane ili

³⁰ Mizanul- Hikma, Juz. 1, Uk. 541.

³¹ Rejea iliyotangulia Juz. 7, Uk. 122.

mwanadamu aweze kubadilisha, lakini taufiki inafuata matakwa ya mwanadamu na hiyari yake, wale wanaochagua wema kwa matakwa yao kwanza Mwenyezi Mungu anawapa taufiki ya mafanikio.

وَالَّذِينَ جَاهَدُوا فِينَا لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبُلَنَا وَإِنَّ اللَّهَ لَمَعَ الْمُحْسِنِينَ

“Na wale wanaofanya juhudi kwa ajili Yetu, hakika tutawaongoza kwenye njia Zetu. Na hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wema.” (Sura Ankabut: 69).

وَالَّذِينَ اهْتَدَوْا زَادَهُمْ هُدًى وَآتَاهُمْ تَقْوَاهُمْ

**“Na ambao wameongoka anawazidishia uongofu.”
(Sura Muhammad: 17).**

Ama ambao hawajachagua uongofu hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi.

أَفَرَأَيْتَ مَنْ اتَّخَذَ إِلَهَهُ هَوَاهُ وَأَضَلَّهُ اللَّهُ عَلَىٰ عِلْمٍ وَخَتَمَ عَلَىٰ سَمْعِهِ وَقَلْبِهِ
وَجَعَلَ عَلَىٰ بَصَرِهِ غِشَاوَةً فَمَنْ يَهْدِيهِ مِنْ بَعْدِ اللَّهِ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ

“Je, umemwona aliyefanya hawaa yake kuwa ndio mungu wake? Basi nani atamwongoza baada ya Mwenyezi Mungu? Hamkumbuki?” (Sura Jathiyah: 23).

Hakika uongofu wa Mwenyezi Mungu kwa mwanadamu unafuata uchanguzi wa mwanadamu, hivyo haisihi kwa mwanadamu kutoa hoja ya kudhibitiwa na ada zake kwa sababu anaweza kutumia silaha ya matakwa dhidi ya ada yake.

Waislamu wa mwanzo walitumia matakwa yao na wakajinasua na

shiriki na wakafuata Uislamu, pamoja na kwamba ada zao za shiriki zilikuwa zimewadhibiti na zikawa sehemu isiyotengana na maisha yao.

Na hawa ambao wanaingia katika Uislamu sasa hivi namna gani wanajinasua na ada zao zinazofanana?

Jarida la *As Shariq al-Usat* limenukuu kabla ya siku kadhaa zilizpita ripoti juu ya fikra za baadhi ya Waislamu ambao walisilimu karibuni na miongoni mwao alikuwa ni balozi wa zamani wa Ujerumani Dr. Murad Haufman, humo limetaja:

“Kwamba katika ujana wake alikuwa ametopea katika kunywa pombe na alikuwa ni mjuzi wa aina zake mbalimbali na alikuwa anadhani ni vigumu sana kwake kuacha pombe na kwamba hawezi kulala vizuri bila ya fundu la pombe!! Lakini alipokinaika na Uislamu na akashikamana na maamrishi yake akajipamba na silaha ya matakwa akashinda ada hiyo ya kimakosa iliyojikita katika maisha yake.”³²

Hakika kuna umuhimu wa kuhudhurisha maana hii kubwa ya kuomba maghofira katika mwezi wa Ramadhani hususan, na katika siku hizi za mwisho za mwezi wa Ramadhan, kwa sababu hivi sasa bado fursa ipo ya kupata baraka za Mwenyezi Mungu na kupata msaada wake katika kutimiza madhumuni na malengo ya kweli kwa mwanadamu ndani ya mwezi huu mtukufu.

³² As Shariqi al- Ausat la tarehe 16/12/1999.

NGUVU YA DUA

Na dua ambazo anazisoma muumini katika mwezi huu mtukufu sio zenyewe kwa dhati yake – kama baadhi wanavyodhani – ndio sababu tosha ya kupata maghofira, bali ni wasila wa kumkumbusha mwanadamu na ukulele wa kumsukuma, na ni mazingira ya kiroho ya mageuzi na mabadiliko, ikiwa kosa lolote linahitaji kubadilishwa basi maamuzi yako ya kubadilisha yawe sasa hivi.

Kwa mfano: Namna gani unaamiliana na swala? Je, unaiswali kwa wakati wake au unaipuza? Na je, unadumu katika swala ya jamaa au hapana? Na ikiwa unaweza kwenda kuhiji umefanya nini katika maamuzi yako ya kwenda kuhiji? Na vipi kuhusu kutekeleza haki za kisharia kama vile khumsi na zaka? Ikiwa hukuwa unaihisabu nafsi yako katika kutekeleza khumsi, basi chukua maamuzi katika siku hizi ili mali zako ziwe twahara na chakula chako na vinywaji vyako viwe halali, na nyumba yako ambayo unaswali humo na mavazi ya kuswalia yawe ya halali, kwani uhalali ni sharti la kusihi swala na hilo halitimii kama hujatekeleza haki za kisharia.

Na katika upande wa kitabia ukoje muamala wako pamoja na familia yako? Je wewe unafanya wajibu wako kwa wazazi wako na mke wako? Ziko wapi sehemu za kasoro na mapungufu?

Na katika uhusiano wa kijamii je, una uadui na yeyote? Na kwa nini unaendelea na uadui na watu wengine kati ya watu wa jamii yako?

Na hata katika ada binafsi kama vile kuvuta sigara na mazoea yasiyofaa kiafya au kiuchumi, ni wajibu wako ujipambe kwa ushujaa katika kuchukua maamuzi ya mageuzi na mabadiliko kuhusiana nayo.

Ugumu wa Maamuzi:

Hakika kusoma Qur'an na kusoma dua zilizopokelewa kutoka kwa Ahlulbaiti (as) na kujua thamani ya muda mtukufu kama vile usiku wa Laitul-Qadir yote hayo yanashajiisha matakwa ya mwanadamu, na yanaamsha ushujaa wake na yanajenga hali ya kujiamini katika nafsi yake, ili achukue maamuzi magumu ambayo kwayo anabadilisha kosa la ada zake na vitendo vyake.

Kama ambavyo mazingira yanayomzunguka mwanadamu ikiwa ni mazuri yana athari kubwa katika kumsaidia katika mabadiliko ya kheri na wema. Na kinyume chake, kama akiwa katika mazingira mabaya na maovu basi maamuzi yake ya mwanzo yawe ni kuyahama na kuepukana nayo.

Tunaomba Mwenyezi Mungu awape wote taufiki ya kutumia fursa ya siku hizi tukufu kwa kuchukua maamuzi ya mabadiliko na kwenda kwenye hali bora zaidi na kama kila mwanadamu miongoni mwetu akichukua hata uamuzi mmoja mwema, na akashikamana nao mwaka mzima basi tungepata kheri nyingi.

Hakika baadhi wanaweza kuamua lakini wanadhoofika na wana-rejea nyuma wakati wa utekelezaji, na baadhi wanashikamana na maamuzi yake kwa muda kisha anapuuza maamuzi na yanayeyuka maamuzi yake, na hii inadhihirisha kwamba haeshimu nafsi yake na wala haithamini.

Imamu as-Sadiq (as) anasema: “Mwenye kufanya kitendo kati ya vitendo vya kheri, basi adumu nacho mwaka mzima na wala asi-katishwe na kitu kingine.”³³

³³ Mizanul-Hikma, Juz. 7, Uk. 17.

NI IDDI YA UPENDO NA USAFI NA SI KUGOMBANA

Ugomvi unakwaza maisha mazuri kwa watu, na unahadaa mazingatio ya jamii, na unapotosha mwelekeo wake. Ambapo ugomvi unateketeza sehemu kubwa katika mazingatio ya mwanadamu. Na katika ugomvi na mzozo mwanadamu anatumia nguvu zake nyingi, fikra na mawazo, na anatumia juhudi na muda wake wa thamani kwa ajili ya kupata ushindi, nguvu ambazo ilipaswa kuzielekeza katika kujenga na kukuza na kuendelea kuelekea kwenye kheri, na kila jamii inapojiepusha na ugomvi na matatizo ya mizozo inaweza kukita juhudi zake kwa ajili ya kupata maslahi mazuri ya jamii na lengo kubwa na zuri.

Mazingira ya Ugomvi:

Ugomvi unaweza kuwa ndio sababu ya kuzifanyia haki uadui au dhana ya kutaka kufanya uadui, ikiwa upande wowote utafanya uadui katika haki za wengine, hakika hilo linachochea kwao utashi wa kutetea nafsi kulipiza uadui, na Uislamu unatia mkazo kuheshimu haki za wengine za kimada na za kimaanawi, na unaharamisha sana uadui au dhuluma yoyote, na ikiwa utatokea ubaya au uadui baina ya wanajamii hakika unashajiisha kusamehe na usamehevu:

فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الظَّالِمِينَ

“Na mwenye kusamehe na kusuluhisha basi huyo malipo yake yapo kwa Mwenyezi Mungu.” (Sura Shura: 40).

وَالْكَافِرِينَ الْغَائِبِينَ عَنِ النَّاسِ وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ

“Na wazuiiao ghadhabu na wenye kusamehe watu na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao ihisani.” (Sura Imran: 134).

Na kutoka kwake (saww): “Sameheaneni mtaondosha chuki baina yenu.”³⁴

Na wakati mwingine sababu ya ugomvi inakuwa ni dhana tu, kwamba upande mwingine umefanya uadui au kwamba pengine utafanya uadui katika siku zijazo, jambo ambalo linaingia chini ya anwani ya dhana mbaya kwa wengine, au kuhisi husuda katika nafasi yao, na kuwa na ghera katika dhati kati yao, anasema Imam Ali (as): “Dhana mbaya inaharibu mambo na inaleta shari.” “Mwenye kushindwa na dhana mbaya hatoacha baina yake na baina ya rafiki suluhu.”

Na inawezekana kuugawa ugomvi na uadui katika aina nyingi:

- Ugomvi wa kidini.
- Ugomvi wa kimaslahi katika kugombania mali au cheo au ladha.

Na nukuu za historia zimekusanya matukio ya umwagaji damu yaliyotokea kwa sababu ya ikhitilafu za kidini na kiitikadi, ingawa wakati mwingine inafichikana chini yake ikhitilafu za kimaslahi za kimaada, na dini itakuwa ni mwelekeo tu au anwani au silaha katika vita.

Ugomvi katika dini:

Je, katika dini kuna yanayopelekea na kutoa kisingizio cha ugomvi? Na kwa maneno mengine je, inajuzu kukhitalifiana kwa sababu za

³⁴ Mizanul- Hikma, Juz. 6, Uk. 367.

kidini na kiitikadi na kutatua ikhitilafu zao hizo kwa vita na mapigano?

Kwa hakika, hakika sisi tunapofuatilia hukumu za kisharia tunakuta kwamba hakuna kisingizio cha ugomvi katika dini kabisa na hiyo ni kwamba:

Kwanza: Hakika dini ni jambo la moyoni na wala hakuna uwezekano wa kuwalazimisha watu itikadi fulani maadamu hawajakinaika nayo. Na Mwenyezi Mungu ameshawaumba watu wakiwa huru na wala hakuwalazimisha wamwamini, na wala hakuruhusu hata kwa Manabii wake kuwalazimisha watu kuamini. **“Hakuna kulazimisha katika dini umeshabainika uongofu na upotovu.”**

فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيِّرٍ

“Kumbusha hakika wewe ni mkumbushaji tu. Wewe si mwenye kuwalazimisha.” (Sura Ghashiyah: 21 – 22).

وَقُلِ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكُمْ فَمَنْ شَاءَ فَلْيُؤْمِنْ وَمَنْ شَاءَ فَلْيُكْفُرْ ۗ

“Sema haki inatoka kwa Mola wako anayetaka aamini na anayetaka akufuru.” (Sura Kahfi: 29).

Pili: Hakika njia pekee inayomruhusu mwanadamu kumkinaisha mwingine kwa yale anayoyaamini na kuona ndio sahihi ni majadiliano na mdahalo, ama uadui na ugomvi hakika sio tu unashindwa kukinaisha upande mwingine, bali unamfanya kuwa adui mkubwa na uwiano unapobadilika basi matokeo pia yanabadilika:

وَلَا تَسْتَوِي الْحَسَنَةُ وَلَا السَّيِّئَةُ ۗ ادْفَعْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ

“Mema na maovu hayawi sawa. Zuia uovu kwa lililo jema zaidi. Mara yule ambaye baina yako na yake pana uadui atakuwa kama rafiki mkubwa.” (Sura Fuswilat: 34).

Na Qur’an tukufu inatia mkazo kwamba mjadala na mdahalo pamoja na Ahlulkitabu ima uwe kwa njia iliyo bora au usifanyike kabisa:

وَلَا تُجَادِلُوا أَهْلَ الْكِتَابِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ قُولُوا
أَمَّا بِالَّذِي أُنزِلَ إِلَيْنَا وَأُنزِلَ إِلَيْكُمْ وَإِلَيْنَا وَإِلَهُكُمْ وَاحِدٌ وَتَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ

“Wala usijadiliane na watu wa Kitabu isipokuwa kwa njia iliyo nzuri kabisa; isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: Tumeamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu. Na Mungu Wetu na Mungu Wenu ni Mmoja na sisi ni wenye kusilimu Kwake.” (Sura Ankabut: 46).

Na anasema (swt):

ادْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحُكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ وَجَادِلْهُمْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ
إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ

“Waite kwenye njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola Wako ndiye anayemjua zaidi aliyepotea njia yake na Yeye ndiye anayewajua zaidi walioongoka.” (Sura Nahli: 125).

Tatu: Ikiwa inajuzu kwako kuwafanyia watu uadui na kugombana nao kwa sababu wameshikamana na kukinai kwao kinyume na kukinai kwako, hakika hilo linamaanisha kwamba wao pia wana haki kuamiliana pamoja nawe kwa njia hiyo hiyo, na ilihali wewe hukubali hilo, na unapenda watu wangeheshimu itikadi yako na

kukinaika kwako, maadamu uko hivyo basi amiliana na watu kwa yale unayopenda waamiliane na wewe.”

Anasema Imam Ali (as): “Ifanye nafsi yako ndio kipimo kwa yaliyo baina yako na baina ya wengine, mpendeele mwingine unayoyapenda kwa ajili ya nafsi yako na chukia kwake unayoyachukia kwa ajili ya nafsi yako.”³⁵

Na kutokana na ukweli huu hakika Uislamu haujaruhusu jihadi na vita pamoja na makafiri isipokuwa katika hali ya kujitetea, kama watawafanyia Waislamu uadui au katika hali ya kuwazuia na kuwakwaza kueneza Uislamu na kulingania imani yao. Na katika yasiyokuwa hayo hakika Uislamu unalingania kwenye muamala mwema pamoja na mwingine, anasema (swt):

لَا يَنْهَاكُمْ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُفَاتِلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ أَنْ تَبَرُّوهُمْ وَتُقْسِطُوا إِلَيْهِمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ

“Mwenyezi Mungu hawakatazi kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakuwapiga vita, wala hawakuwatoa makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu. “
(Sura Mumtahirah: 8).

³⁵ Nahjul-Balagha, barua ya 31, Uk. 397.

KATIKA DUARA LA UISLAMU

Na ikiwa kugombana na watu wa dini zingine inakatazwa, basi suala hilo la kugombana na watu wa madhehebu mengine katika dini moja inafaa lipingwe kabisa, ambapo anwani ya Uislamu inawaenea wote na “Kila mwislamu kwa mwislamu mwingine ni haramu mali yake, damu yake na heshima yake.”³⁶

Bali kinachotakiwa kwa watu wa madhehebu zote wafunguke na kuwa wawazi kwa madhehebu mengine, na Maimamu wa Ahlulbait wamewafundisha adabu wanafunzi wao juu ya hilo.

Kutoka kwa Muawiya bin Wahab amesema: Nilimwambia Imam Ja’far as-Sadiq (as): Namna gani inatupasa tufanye baina yetu, baina ya watu wetu na baina ya wengine miongoni mwa watu kati ya wale ambao hawako katika jambo letu? Akasema: “Mtawatazama Maimamu wenu ambao mnawafuata na mtafanya wanayoyafanya, wallahi hakika wao wanawatembelea wagonjwa wao na wanasindikiza jenza zao na wanatoa ushahidi kwao na kwao wanatekeleza amana.”³⁷

Na duara finyu sana ndani ya duara la Uislamu ni duara la madhehebu, ambapo inaweza kukawa na makundi na mirengo mingi ndani ya madhehebu moja, katika madhehebu ya Ja’fari kwa mfano kuna tofauti baina ya *Akhbariyina* na *Usuliyina* katika mfumo wa kung’amua hukumu za kisharia na kuna ikhithilafu baina ya *Shai-khiya* na wengineo katika baadhi ya rai zinazofungamana na nafasi ya Ahlulbait (as), kisha kuna mafungamano ya kisiasa na kijamii na kuwepo Marjaa wengi wa kukalidiwa.

³⁶ Muslimu bin al- Hajaj al-Qarashiy Anisaburiy katika Sahihi Muslim, Chapa ya kwanza 1998, Riyaadh (Darul- Mughuniy) Hadithi namba: 2564.

³⁷ Muhammad bin Yaaqub al- Kulainiy katika al- Kaafiy, Juz. 2, 1405 A.H (Beirut Darul adhuwaai) Uk. 136.

Lakini ikhitilafu hii na tofauti hii haisihi abadani iwe ni kisingizio cha ugomvi na uadui baina ya watu wa madhehebu moja na dini moja.

Hakika jamii inapokuwa inashikamana na adabu za Uislamu na inajua madhara ya ugomvi juu yake, na inapokuwa imepevuka katika muamala wake pamoja na taklifu zake za kisharia hakika itabadilisha kila mas'ala yenye ikhitilafu ya kielimu juu yake na kuwa ni nukta yenye nguvu inayoongezwa katika hazina yake, na sio kiungo cha kulipua na matatizo.

Na mbele yetu kuna mifano ya ikhitilafu katika kuthibiti mwezi, nayo ni mas'ala siku hizi yamekuwa ni mazingatio ya wananchi wote wa nchi za Kiislam, ambapo inawezekana sana baadhi ya dola za Kiislamu kutangaza Iddi katika siku hii na dola nyingine katika siku nyingine.

Na hata ndani ya madhehebu moja inawezekana kutofautina rai katika kuthibiti mwezi au kutohibiti kwake. Je, inasihhi mfano wa ikhitilafu hii kuwa ni sababu ya ugomvi au mzozo ndani ya jamii?

Mtazamo wa Kifiqihi:

Ili kutatua maudhui haya ni lazima tutaje utangulizi. Nayo ni kwamba mbele ya mukalafu kuna kauli dhahiri ya kufunga katika hali ya kutohibiti mwandamo wa mwezi wa Shawwali, na kufungua inapothibiti kuandama kwake. Na maadamu hayajapatikana matumaini ya kuthibiti mwezi mwandamo haijuzu kwake kufungua bali ni juu yake kukamilisha idadi ya siku thelathini.

Na ama matumaini ya kuandama mwezi yanapatikana kwa moja ya njia za kisharia zilizotajwa katika vitabu vya kifiqihi, nazo ni mtu mwenyewe kuona mwezi au waadilifu wawili kushuhudia, au kunea habari (ya kuandama mwezi) kwa tawatur.

Na kwa kuwa hukumu inategemea kupatikana kwa matumaini kupitia moja ya njia zilizotajwa, hivyo kama yatapatikana kwa njia yoyote kati ya hizi inathibiti kwa mukalafu hali ya kuwajibika kwa kufuata athari yake.

Na kwa kuwa mukalafu wengi aghlabu hawaoni mwezi, kama ambavyo sio rahisi kila mmoja kusikia ushahidi wa mashahidi wawili waadilifu wa kuonekana kwake, na inawezekana zisienee kwa walio wengi, kwa hiyo watu wamezoea kutegemea rai ya maulamaa wanaoshughulikia jambo hili, ambao wao ndio sehemu ya matumaini yao na uaminifu wao, na anapothibitisha mwanachuoni ambaye anatumainiwa, hakika watu wanaomwamini wanafuata kauli yake.

Na hapa ni wajibu kutilia mkazo juu ya mambo mawili muhimu sana:

Kwanza: Kila mukalafu anapofuata athari ya kisharia inayotokana na matumaini yake au kutopata matumaini haijuzu katika hali ya kukhitalifiana kumfanyia uadui huyu na yule au kinyume chake, kwa sababu pande zote mbili zimefanya kulingana na taklifu yake ya kisharia, na kulazimiana na hukumu ya kisharia katika mas'ala, hivyo haijuzu kuwa ni sababu ya ugomvi, kama mtu atamkaribisha msafiri katika nyumba yake na akaswali kwa kupunguza swala haijuzu kwa mwenye nyumba kumfanyia uadui kwa hilo, na hata kama jamaa watakhitalifiana kuainisha upande wa kibla na kila mmoja miongoni mwao akaswali kwa kuelekea upande anaotakidi au anaodhani ndio kibla haijuzu hilo kuwa ni sababu ya ugomvi. Ndio inawezekana kila mmoja wao kubainisha sababu ya kushikamana kwake na rai hii bila ya ile, pamoja na kuchunga adabu ya mjadala kulingana na ikhitalafu.

Pili: Hakika watu kutegemea rai ya maulamaa katika kuthibiti mwezi au kutothibiti kwake ni kwa sababu wao wanaweza

kutekeleza vipimo vya kisharia, isipokuwa ni kwamba hilo halisihi kuwa ni sababu ya kugeuza kitendo cha kuthibiti mwezi mwandamo au kupinga kwake kuleta hali ya mgawanyiko, kila kundi litachukua rai ya mwanachuoni ambaye wanaelemea kwake, pamoja na kufumbia macho mtazamo wa wanachuoni waliobaki.

Na hii haiwezi kutimia isipokuwa ikiwa huyu mwanachuoni ndio pekee katika mtazamo wao ambaye rai yake inaweza kuleta matumaini, ama mwinginewe kati ya maulamaa hana thamani katika maneno yao.

Hakika haisihi kugeuza mas'ala haya ya kisharia kuwa ni kadhia ya mgawanyiko, yanapopatikana matumaini kwa mukalafu ya mwandamo wa mwezi wa Shawwali kwa uthibitisho wa mwanachuoni yeyote mwaminifu kwake, ni wajibu juu yake kumfuata katika hilo, na ikiwa hajapata matumaini ya kuthibiti kwake basi hatofuata na hata kama aliyemthibitishia ni Marjaa anayekalidiwa, hakuna mafungamano baina ya Marjaa anayekalidiwa na mukalafu katika kadhia hii ya kimaudhui, mukalafu anaweza kupata matumaini kwa moja ya njia za kisharia na kufungua wakati ambapo Marjaa wake amefunga, na anaweza kuwa kinyume cha hivyo. Na hata katika kujengea juu ya nguvu ya utawala wa kisharia kwa mwandamo wa mwezi hakika hiyo inashurutishwa kwamba asijue mukalafu kosa la mtawala wa kisharia wala kosa la tegemeo lake katika hukumu yake ya mwandamo wa mwezi.³⁸

Iddi ya Upendo na Usafi:

Hakika inatakikana sote tufanye juhudi ili Iddi iwe ni mnasaba wa kusambaza hali ya upendo na usafi, na kuzatiti upendo na udugu baina ya waumini na Waislamu. Hivyo ni muhimu kujongea katika mambo yafuatayo:

³⁸ Imamu Ruhullah al- Musawiy al- Khumainiy katika Taharir al-Wasilah, Juz. 1, 1424 A.H (Beirut Daru Taarifu Lilimatubuati), Uk. 265.

1. Kuzingatia na kufuatilia mwandamo wa mwezi kwani ni suna kufanya hivyo, na inapasa kudumu katika hilo kwani kila inapozidi idadi ya wanaotazama mwezi basi fursa ya kuona mwezi mwandamo inakuwa kubwa zaidi katika usiku wa kuandama mwezi.
2. Mwenye kuona mwezi mwandamo kutoa ushahidi wake mbele ya wanachuoni wanaohusika katika nchi yake wala wasizembe na kwenda kwa baadhi yao bila ya kuwashirikisha wengine, ili wanachuoni wote wanaohusika wawe katika mazingira yanayokaribiana yanayosaidia katika msimamo mmoja.
3. Tuwasukume na tuwashajiishe kukutana maulamaa wanaoshughulika na kuthibitisha mwezi mwandamo pamoja na baadhi yao na washauriane baina yao ili kuchukua msimamo mmoja utakaowapa raha watu kutokana na taabu ya ikhitilafu.
4. Kila upande uheshimu rai ya upande mwingine wakati wa kuhitalifiana katika kuthibiti mwezi, atakayefungua au kufunga hiyo ni taklifu yake ya kisharia baina yake na baina ya Mola wake, na wala haisihi kutuhumu niya, wala kuwa na dhana mbaya, wala kufanya uadui juu ya haki za wengine na kupaka matope shakhisiya zao au uchochezi dhidi yao.
5. Kueneza utamaduni wa kusameheana, na mafunzo ya Uislamu katika maingiliano mazuri na kuamiliana pamoja na watu hata kama wametofautina katika dini zao na madhehebu yao na rai zao na mielekeo yao, kuna hadithi nyingi zilizopokewa kutoka kwa Maimamu watoharifu (as) zinazokatata ugomvi katika dini, wala sijui ni kwa nini tunasa-

hau hadithi hizi na wala hatuelezani pamoja na kuzihitajia sana.

Imepokewa kutoka kwa Imam Ja'far as-Sadiq (as): “Msigombane na watu kwa ajili ya dini yenu hakika ugomvi unatia ugonjwa katika moyo.”³⁹

Na kutoka kwake (as): “Jihadharini na ugomvi katika dini hakika unashughulisha moyo na kuzuia utajo wa Mwenyezi Mungu mtukufu na unarithisha unafiki na unaleta chuki.”⁴⁰

Na kutoka kwa Ali bin al-Yaqitwin amesema: Amesema Abu Hasan Imam Musa bin Ja'far (as): “Waamuru wafuasi wako wazuie ndimi zao na waache ugomvi katika dini na wajitahidi katika kumwabudu Mwenyezi Mungu mtukufu.”⁴¹

Na katika riwaya hizi kuna ishara ya madhara ya ugomvi katika dini nayo ni:

1. Unamuudhi mwanadamu kinafsi (unaleta maradhi katika moyo)
2. Unasababisha chuki na uadui katika jamii (unaleta chuki).
3. Unamzuia mwanadamu na mazingatio halisi (unashughulisha moyo na kuzuia utajo wa Mwenyezi Mungu).

³⁹ Biharul- An'war, Juz. 2, Uk. 133.

⁴⁰ Rejea iliyotangulia, Uk. 128.

⁴¹ As Suduq Muhammad bin Ali bin Babawayhi al-Qummiy, katika Tauhid (Beirut Darul-Maarifah) Uk. 460.

REJEA

1. Qur'an Tukufu
2. Ibnu Babawayhi al- Qummiy: As Suduqu Muhammad bin Ali katika Tauhidi, Darul- Ma'arifah.
3. Al- Amadiy Tamiymiy: Abdul- Wahdi katika Ghuriril- Hikami wa Duraril- Kalimi, Chapa ya kwanza 1987 Muasatul- Ilmiy Lilimatubuati, Beirut.
4. Tirmidhiy: Muhammad bin Isa bin Surah Katika Sunan Tirmidhiy, Chapa ya kwanza 2000 Darul- Kutubil- Ilimiyah, Beirut.
5. Al- Hurrul- Aamily: Muhammad bin al- Hasan katika Wasailu Shia, Chapa ya kwanza 1993, Muasatu Ahlulbait Liihiyai Turathi, Beirut.
6. Al- Huwaiziy katika Tafsir Nuru Thaqalain, Chapa ya nne 1412 A.H, Muasatu Ismailiyan, Qum.
7. Raishahariy: Muhammadiy katika Mizanul- Hikmah, Markaz Nashir Maktabil- Ilaamiy, Qum.
8. As Shariq al- Ausat 16/12/1999.
9. As-Shariq: Majalatu Usubuiyah, linalotolewa na Muasatu Shariqiya Lilitwiba'ati wa Swahaafati wal-Iilaami, toleo la 999.
10. As-Swaawiy: Dr. Abdul- Jawad, katika Swiyaam Mu'ujizati Ilimiyah, Chapa ya kwanza 1993 Darul- Qiblah, Jiddah.

11. Al- Fakhariy Razi: katika Tafsirul- Kabir, Chapa ya tatu ya Daru Ihiyail- Turathi al- Arabiy, Beirut.
12. Al- Qashiyriy an-Nisaburiy: Muslim bin al- Hajaj katika Sahih Muslim, Chapa ya kwanza 1998, Darul- Mughuniy, Riyaadh.
13. Al- Kulaiyniy: Muhammad bin Yaaqub, katika al- Kaafiy, Daru al- Adhuwai 1985, Beirut.
14. Al- Majilisiy: Muhammad al-Baaqir, katika Biharul- An'war, Chapa ya pili 1983 Daru Turathil- Arabiy, Beirut.
15. Al- Musawiy: Sharif Ridhaa katika Nahjul- Balagha, kimehakikiwa na Dr. Swabahiy Swalehe, Chapa ya kwanza 1967 Darul- Kitabil Libnaaniy Beirut.
16. Al- Hindiy: Ali al-Mutaqiy, katika Kanzul- Ummali, Chapa ya tano 1985, Muasastu Risalah, Beirut.

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. i) Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
ii) Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (a.s.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua kwa Mujibu wa Ahlulbayt (a.s)
33. Udhuu kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Qur'ani na Kuhifadhiwa Kwake
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya Sala Mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an Yatoa Changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Eلفu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Eلفu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Eلفu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Eلفu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Eلفu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Eلفu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-Ilaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Dhana ya Ndoa ya Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raj'ah)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema

89. Adabu za Sokoni Na Njiani
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali (AT- TAWASSUL)
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunna za Nabii Muhammad (saww)
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Mwanamke Na Sharia
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqaalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne

120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul l'Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
136. Tabaruku
137. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mjadala wa Kitiikadi
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu

151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Shia na Qur'ani – Majibu na Maelezo
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. as-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)

182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Historia maana na lengo la Usalafi
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji Dhahiri katika (Turathi) Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (as) na Makhaliifa
197. Tawheed Na Shirki
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni waKisunni na Kishia (Al- Muraja'aat)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebicho na Mageuzi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza

213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahju ‘L-Balagha– Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Mazingatio Katika Swala
223. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
224. Vyakula Na Vinywaji
225. Kuelewa Rehema ya Mwenyezi Mungu
226. Imam Mahdi na Bishara ya Matumaini
227. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
228. Shia Na Sahaba - Majibu na Maelezo
229. Majanga Na Jukumu la Jamii
230. Shia Na Hadith - Majibu na Maelezo
231. Upotofu Ndani ya Kitabu cha Mitaala kwa Shule za Sekondari
232. Ugaidi Wa Kifikra Katika Medani Ya Kidini
233. Yafaayo kijamii
234. Uswalihina Dhahiri Na Batini Yake
235. Mkakati wa Kupambana na Ufakiri
236. Mwanamke Katika Harakati Za Mageuzi
237. Jihadi
238. Hija Katika Maneno Na Ujumbe Wa Imam Khomeini (R.A)
239. Tiba Ya Maradhi Ya Kimaadili
240. Yusuf Mkweli
241. Taqiyya Kwa Mujibu Wa Sheria Ya KIISLAMU

242. Imam Mahdi (A.S) Imam Wa Zama Hizi Na Kiongozi Wa Dunia
243. Talaka Tatu
244. Safari Ya Kuelekea Kwa Mwenyezi Mungu
245. Hotuba Za Kiislamu Juu Ya Haki Za Binadamu
246. Mashairi Ya Kijamii
247. Ngano Ya Kwamba Qur'ani Imebadilishwa
248. Wito Kwa Waumini: "Enyi Mlioamini"
249. Imam Husain (a.s) ni Utu na Kadhia
250. Imam Husain ni Kielelezo cha Kujitua Muhanga na Fidia
251. Imam Mahdi ni Tumaini la Mataifa
252. Kuchagua Mchumba
253. Mazungumzo ya Umoja – Ukosoaji na Usahihishaji
254. Utamaduni wa Mwamko wa Kijamii
255. Hekima za kina za Swala
256. Kanuni za Sharia za Kiislamu
257. Utamaduni kufuatana na Qur'ani na Utekelezaji wa Kivitendo (Sehemu ya Kwanza)
258. Kauli sahihi zaidi katika kufafanua Hadithi